

Kutoa majibu

Tunaamini kwamba umefurahia huduma uliyopokea leo – kama ungependa kuacha maoni yoyote, mawazo au mapendekezo kuhusu programu yetu, kadi za majibu zinapatikana kwenye eneo la kliniki la mapokezi au unaweza kutupigia simu nambari 13 20 50.

Ushuhuda

Kama ungependa kushiriki hali yako nzuri uliyopitia katika BreastScreen SA na wanawake wengine ili kuwahimiza kushiriki katika uchunguzi wa saratani ya matiti, tungependa kusikia kutoka kwako! Kuna mseto wa njia unazoweza kutoa hadithi yako – tafadhali wasiliana na kundi la Uhamasishaji na Elimu katika nambari 08 8274 7100 au baruapepe BSSApromoed@health.sa.gov.au ili kupata kujua zaidi.

Tunatazamia kukuona tena wakati wa uchunguzi wako unaofuata wa matiti.



For more information

BreastScreen SA
SA Health
Telephone: 13 20 50
www.sahealth.sa.gov.au/breastscreen
bssaenquiries@health.sa.gov.au

If you do not speak English, request an interpreter from SA Health and the Department will make every effort to provide you with an interpreter in your language.



www.ausgoal.gov.au/creative-commons

© Department of Health and Ageing, Government of South Australia. All rights reserved. Printed March 2014. 13038

Baada ya
miadi yako
ya uchunguzi
wa matiti

Nini hufanyika baada ya uchunguzi wangu wa mamogramu?

Picha zako za uchunguzi wa mamogramu zitatumwa katika Kitengo chetu cha Mratibu wa Jimbo kule Adelaide ili kuchunguzwa kwa njia huru na angaa wataalamu wawili madaktari (wanarediolojia).

Nitapokea matokeo yangu lini?

Kama hakutakuwa na ishara za saratani ya matiti au utathmini wowote wa ziada utakaohitajika wewe pamoja na daktari wako mteule mtafahamishwa kuhusu matokeo yako kwa maandishi kwa muda wa siku 14.

Wanawake wengi wamehakikishiwa tena kwamba picha zao hazina ithibati yoyote ya saratani ya matiti.

Picha zako za uchunguzi wa matiti zitahifadhiwa katika BreastScreen SA ili ziweze kupatikana kwa ulinganisho na uchunguzi wako wa siku za usoni. Kama umeleta picha za binafsi, zitarudishwa kwako.

BreastScreen SA ina sera kali za faragha na wafanyikazi wetu hawawezi kuacha ujumbe wa simu au kujadili matokeo yako na wanauko wako au wengine bila ya idhini yako.

Tafadhali wasiliana na BreastScreen SA kama haujapokea matokeo yako kwa muda wa siku 21.

Je, itakuwaje kama vipimo zaidi vinahitajika?

Idadi ndogo ya wanawake watahitajika kurudi kwa kufanyiwa vipimo zaidi. Hivi vinaweza kujumuisha picha zenye maelezo zaidi za Eksirei, uchunguzi wa kipimo cha matiti na vipimo vingine vinavyofanywa bila malipo katika Kliniki yetu ya Utathmini kule Adelaide.

Wanawake wengi wanaoitwa kwa utathmini na vipimo zaidi wanahakikishiwa tena kwamba hawana saratani ya matiti.

Tafadhali unaombwa kupatikana kwa wiki sita baada ya miadi yako ya uchunguzi wa matiti endapo kutakuwa na vipimo zaidi vinavyohitajika.

Kama unapanga kuondoka, tafadhali tupatie maelezo ya anwani mbadala tunayoweza kutumia.

Je, uchunguzi wangu unaofuata wa matiti utakuwepo lini?

Kama hakutakuwa na ishara za saratani ya matiti, utatumiwa kumbusho la kukualika katika uchunguzi wako unaofuata wa matiti kwa muda wa miaka miwili ijayo. Katika kesi fulani, uchunguzi wa kila mwaka wa matiti unaweza kupendekezwa.

Kufanyiwa uchunguzi wa matiti hauzuii saratani ya matiti katika siku zijazo na uchunguzi wa matiti unahitaji kurudiwa katika awamu za mara kwa mara ili kugundua mabadiliko ya matiti.

Ninaweza kufanya chochote kingine kati ya ziara zangu za kuwatembelea ili kufanyiwa uchunguzi?

Kati ya ziara zako za kufanyiwa uchunguzi, ni muhimu kwako kujua mtazamo wa kawaida na kuweza kuhisi matiti yako. Kama utagundua mabadiliko, kama vile dude au usaha kutoka kwenye chuchu unafaa kuwasiliana na daktari wako haraka iwezekanavyo ili kupanga uchunguzi zaidi.

Nini hufanyikia taarifa inayohusu ziara yangu ya uchunguzi?

Matokeo ya vipimo vyovyote ulivyonavyo na nakala za picha za uchunguzi za matiti kama itahitajika zitaweza kutumwa kwa daktari wako teule, na kwa daktari wengine yeyote wanaohusika katika vipimo zaidi au matibabu. Taarifa kuhusu uchunguzi wowote na matibabu yanayofuata uchunguzi wako wa matiti hukusanywa kutoka kwa madaktari wako wanokutibu ili kusaidia BreastScreen SA katika kuhakikisha kwamba unapokea utunzaji unaofaa zaidi.

Ninawezaje kufikia rekodi zangu?

Nakala za picha zako za uchunguzi wa matiti zinaweza kupatikana, kwa kibali chako, kwa huduma yoyote nyingine ya BreastScreen Australia ambayo umehudhuria. Zitaweza pia kutolewa kwa mtaalamu(wa) wako mteule(wa) kama atahitajika kwa matibabu yanayoendelea.

Nakala za faili yako kwa rekodi zako za kibinafsi zinaweza kupatikana kwa kuandikisha ombi la Uhuru wa Taarifa. Unaweza pia kuhitajika kulipia ada. Ili kupata kujua zaidi tafadhali wasiliana na BreastScreen SA katika nambari 13 20 50.